



# NCHI YETU

Jarida la Mtandaoni



TOLEO NA.3

Limeandaliwa na Idara ya Habari-MAELEZO

TOLEO LA MACHI 2017

## MWAKA WA FEDHA 2017-2018: BAJETI YA MAENDELEO JUU

- Miradi saba mikubwa ya kipaumbele kutekelezwa
- Lengo ni kufikia malengo ya Dira 2025



# Bodi ya Uhariri

## Mwenyekiti

Dkt. Hassan Abbasi

*Mkurugenzi-Idara ya Habari-MAELEZO*

## Wajumbe

Zamaradi Kawawa

Vincent Tiganya

John Lukuwi

Elias Malima

## Msanifu Jarida

Hassan Silayo

## Huduma zitolewazo MAELEZO

1. Kuuza picha za Viongozi wa Taifa na matukio muhimu ya Serikali.
2. Kusajili Magazeti pamoja na Majarida
3. Kukodisha ukumbi kwa ajili ya mikutano na Waandishi wa Habari.
4. Rejea ya Magazeti na Picha za Zamani
5. Kupokea kero mbalimbali za wananchi.

## Jarida hili hutolewa na:

*Idara ya Habari-MAELEZO*

S.L.P 8031

*Dar es Salaam-Tanzania*

*Simu : (+255) 22 -2122771*

*Baruaapepe:maelezo@habari.go.tz*

*Tovuti: www.maelezo.go.tz*



**WATUMISHI HOUSING COMPANY**  
"Dhamana ya Uwekezaji katika Nyumba"



## “Hamia kwako leo”

kwa mkopo wa nyumba wa bei nafuu.

Malipo ni ndani ya mwaka 1 hadi miaka 25.

Kwa sasa tunajenga na kuuza nyumba bora na kisasa maeneo mbalimbali nchini:

Kigamboni (Gezaulole)	Mwanza (Kisesa)
Morogoro (Mkundi)	Bunju B (Mabwepande Road)
Magomeni (Usalama Apartments)	

## PIGA SASA

0715 353 465 / 0757 437 594 / 0756 447 422



Kwa maelezo zaidi na kuweza kuchukua fomu za kununua nyumba tembelea ofisi zetu zilizopo jengo la Golden Jubilee Towers gholofa ya 4 au tembelea tovuti yetu.



## TAHARIRI

### **UJENZI BARABARA YA JUU UBUNGO MFANO WA MTAZAMO WA KIMAENDELEO WA JPM**

---

Miundombinu bora ni kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi. Kwa kipindi kirefu jiji la Dar es Salaam limekuwa likikabiliwa na changamoto ya msongamano mkubwa wa magari kiasi kwamba watumishi wa Serikali na wananchi wengine kwa ujumla hutumia wastani wa saa 3 hadi 6 kwenda na kurudi kazini.

Muda huu ni mwingi sana kuupoteza kila siku. Kwa hesabu za haraka huu ni muda mwingi kwa siku, kwa mwezi na hata kwa mwaka. Muda huu ungetumika katika uzalishaji, basi nchi yetu ingepiga hatua kubwa kiuchumi.

Niayawaziya Rais John Pombe Magufuli kuendeleza ujenzi wa barabarazajuu (flyovers) inataraji kupunguza ama kuondoa changamoto hii. Tumeshuhudia hivi karibuni ujenzi wa barabara za juu katika eneo la Tazara ukiendelea ili kupunguza msongamano.

Kuanza kwa ujenzi wa Ubungo nako kutakuwa ni hatua nyingine muhimu na ni wazi kuwa hizi ni juhudini kubwa za Serikali ya Awamu ya Tano katika kuboresha miundombinu ya jiji la kibiashara la Dar es Salaam ambazo hazina budi kupongezwa.

Ujenzi huu ukikamilika, ule msongamano wa kila siku kwa magari yanayotoka maeneo ya jiji kama Buguruni, Uwanja wa Ndege na maeneo ya Gongo la Mboto, Temeke na Posta kuelekea Tazara hautakuwepo tena kwani kila njia itakuwa na eneo lake la kupishana magari bila kusubiriana. Hakika adha ya msongamano itapungua katika maeneo tajwa na hivyo kuharakisha usafirishaji na maendeleo kwa ujumla.

Katika suala hili tumemsikia Rais Magufuli akisema kuwa mradi huo utasaidia kuondoa kero mbalimbali za msongamano, vifo na mambo mengi mengi yaliyokuwa yanakwamisha kutokana na foleni. "Msongamano ni tatizo. Tunataka suala la msongamano kulimaliza na kama si kulimaliza basi kulipunguza," alieleza Rais Magufuli wakati wa uwekaji jiwe la msingi la ujenzi huo.

Akieuzea mradi huo, Rais Magufuli amesema ujenzi utachukua miezi 30 kukamilika na utagharimu jumla ya shilingi bilioni 188 ambapo kati ya hizo bilioni 186 zinazotolewa na Benki ya Dunia (WB) na zingine zitatolewa na serikali ya Tanzania.

Aidha Fly-Over ya Ubungo itakuwa na ghorofa (njia) tatu: njia ya chini, ya katina juu. Njia ya chini itakuwa ni ya Morogoro – Mjini Katavi, Barabara ya juu itakuwa ni kwa ajili ya gari za Mwenge – Tabata huku njia ya katni itakuwa makutano kwa wanaohitaji kubadili njia.

Ni matumaini yetu kuwa miradi hii mikubwa itawanufaisha wananchi wengi bila kujali vyama wala itikadi zao. Kwa kuwa pia jiji la Dar es Salaam litabadilika na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kutokana na kuondokana na msongamano wa magari hivyo kukuza uchumi kwani muda mwingi utatumika katika shughuli za uzalishaji mali, mradi huu uungwe mkono na wapenda maendeleo wote.



**Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni Hodhi Miliki ya Rasilimali za Reli (RAHCO), Masanja Kadogosa (wa tatu kutoka kulia waliokaa), akisaini Mkataba wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli ya Kisasa (Standard Gauge) na wawakilishi wa Makampuni yatakayojenga reli hiyo jijini Dar es Salaam.**

## Na Said Ameir

Serikali, katika mwaka wa fedha ujao wa 2017/2018, imeongeza bajeti ya maendeleo kutoka shilingi bilioni 11,820.5 mwaka 2016/17 hadi shilingi bilioni 11,999.6 ambapo katika mwaka ujao wa fedha Serikali imepanga kukusanya na kutumia shilingi bilioni 31,699.7.

Akiwasilisha Mapendekoko ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na ya Kiwango na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa wabunge, Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Philip Mpango alieleza kuwa kiwango hicho inakwenda

sambamba na matakwa ya Awamu ya Pili ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2016/17 – 2020/21 ambao unaelekeza Serikali kutenga bajeti ya maendeleo kati ya asilimia 30 na 40 ya bajeti yote.

Katika hotuba yake hiyo Waziri wa Fedha aliwaeleza wabunge kuwa Serikali imepanga kutekeleza miradi saba ya kipaumbele ambayo ni mahsus kwa kuwa inatarajiwa kutoa matokeo makubwa kuendana na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Aliitaja kuwa ni Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga, Ujenzi wa Reli ya Kati na Kuboresha Shirika la

Ndege Tanzania, Ujenzi wa Mitambo ya Kusindika Gesi Kimiminika Lindi, Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi, Uanzishwaji wa Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi; na Ununuzi na Ukarabati wa Meli kwenye Maziwa Makuu.

Dk. Mpango alifafanua kuwa katika uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi, Kituo cha Biashara cha Kurasini kimetangazwa kwa wawekezaji tangu mwaka 2016 na eneo la Uwekezaji la Bagamoyo lenye ekari 2,339.6 liko katika hatua mbali mbali za matayarisho huku ekari 110 kati ya hekta 2600 za eneo Maalum la Uwekezaji la Mtwara kwa ajili ya matumizi ya bandari huru (Freeport



**Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwasilisha Mapendekozo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Kiwango cha Ukomo wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha, 2017/18 ambapo imepanga kutumia Sh. Trilioni 31.6.**

Zone) na tayari maandalizi ya kuweka miundombinu, hususan barabara, kwa eneo hilo yanaendelea.

Pamoja na miradi hiyo, Waziri wa Fedha aliongeza kuwa, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mingine ya kipaumbele ikiwemo ujenzi wa Uchumi wa Viwanda ambaa utahusisha uendelezaji wa Eneo la Viwanda, Kufungamanisha uchumi na maendeleo ya Watu na Mazingira Wezeshi ya Uendeshaji Biashara.

Miradi mingine ni uimarishaji wa mitaji na kutumia benki za ndani za maendeleo kama vyombo vya kupanua upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na nafuu kwa wawekezaji; na kuhamishia

shughuli za Serikali Kuu Makao Makuu Dodoma.

Waziri Dk. Mpango alieleza kuwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 ni wa pili katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na dhana yake kuu ni "Kujenga Uchumi wa Viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu".

Kuhusu ukomo wa bajeti, Dkt. Mpango alieleza mkutano huo wa Bunge ambaa ulikuwa chini ya uenyekiti wa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na kuhudhuriwa pia na Spika Job Ndugai na Naibu Spika Dk. Tulia Ackson kuwa Serikali inapendekeza bajeti ya shilingi

trilioni 31.7 ikilinganishwa na shilingi trilioni 29.5 ya mwaka wa fedha uliopita.

Dkt. Mpango alisitiza kuwa mapendekozo hayo ya kiwango na ukomo wa Bajeti ya mwaka 2017/18 yana lengo la kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kuondoa vikwazo vya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya viwanda.

Waziri wa Fedha alibainisha kuwa Serikali, katika mwaka ujao wa fedha, inakusudia kuongeza mapato ya ndani hadi kufikia asilimia 15.9 ya Pato la Taifa ili kupunguza nakisi katika bajeti yake.



## Barabara za Juu Ubungo Kugharimu Shilingi Bilioni 188.71.

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli na Rais wa Benki ya Dunia Dkt. Jim Yong Kim wakifunua kitambaa kuashiria uwekaji wa jiwe la Msingi katika mradi wa ujenzi wa Barabara za Juu katika makutano ya Ubungo jijini Dar es Salaam, Kulia ni Mke wa Rais Magufuli Mama Janeth Magufuli.**

### Na. Immaculate Makilika

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kushirikiana na Rais wa Benki ya Dunia Dkt. Jim Yong Kim hivi karibuni wameweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara za juu (Ubungo interchange), katika makutano ya Ubungo yaliyopo barabara ya Morogoro jijini Dar es Salaam.**

Mradi huo ambao utagharimu takribani shilingi bilioni 188.71 unaotarajiwa kukamilika ifikapo Septemba 2019 ambapo takribani magari 65,000 yatatumia barabara hizo zenyetengenzo la kupunguza msongamano wa magari katika barabara za Morogoro, Nelson Mandela na Sam Nujoma.

Mradi huu ni sehemu ya uboreshajiwa usafiri jiji ni Dar es Salaam yaani Dar es Salaam urban transport improvement project, utakaogharimiwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia na mchango wa Serikali ya Tanzania.

Mh. Rais anasema mradi huo utahusisha pia awamu ya tatu na ya nne ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi ya endayo haraka (bus rapid transit- BRT), katika barabara ya Nyerere kutoka katikati ya jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto na barabara ya Bagamoyo kutoka katikati ya jiji hadi Tegeta.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Rais Magufuli anasema Serikali inalenga kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha

usafirishaji na kuchochea mapinduzi ya viwanda, ambapo ujenzi huo utasaidia kutatua msongamano wa magari katika barabara za Morogoro, Sam Nujoma na Mandela na kuwapatia ajira wakazi wa maeneo ya jirani"

Naye Rais wa Benki ya Dunia Dkt. Jim Yong Kim anasema mradi huo wa mabasi ya endayo haraka ni mfano mzuriwa ushirikanwa Serikali, Sekta binafsi, na Benki ya Dunia itaendelea kushirikiana na Tanzania katika miradi mbalimbali ili kuboresha maisha ya wananchi pamoja na kukuza uchumi wa nchi.

Sambamba na hilo, Dkt. Kim amepongeza utendaji wa Rais Magufuli na kusema kuwa Benki ya Dunia imefurahishwa kuona maendeleo mazuri ya miradi mbalimbali

inayoendelea nchini kwa ufadhili wa Benki hiyo. Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya China Civil Engineering Construction Cooperation (CCECC) Jiang Yigao na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini TANROADS, Mhandishi Patrick Mfugale wamesaini mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo ambapo serikali tayari imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.1 kilicholipwa kama fidia kwa wananchi walioguswa na mradi huo. Mradi huo wa ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo unatarajiwa kuanza hivi karibuni ambapo utasaidia kuokoa muda ambaa wasafiri wamekua wakitumia



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jophn Pombe Magufuli na Rais wa Benki ya Dunia Dkt. Jim Yong Kim wakiwaaga wananchi waliohudhuria hafla ya uwekaji wa jiwe la Msingi katika mradi wa ujenzi wa Barabara za Juu katika makutano ya Ubungo jijini Dar es Salaam.*

katika msongamamo wa mbalimbali za jiji, pamoja na kuwaondolea kero mbalimbali kwa wasafiri.

## **Watanzania kunufaika na gesi asilia ifikapo 2020.**

### **Benjamin Sawe**

Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) imesema mpaka kufikia mwaka 2020 litawawezesha watanzania kutumia gesi majumbani mwao hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira nchini.

Kaimu Mkurugenzi wa TPDC Mhandisi, Kapuulya Musomba anasema muda mrefu kumekuwa na uharibifu wa mazingira hivyo kupatikana kwa nishati ya mafuta na gesi kutaiwezesha Tanzania kuwa mahali salama kimazingira ikiwa ni pamoja na ukuaji wa sekta ya uchumi. Anasema katika robo ya



*Baadhi ya mitambo ya kuchakata gesi katika kituo cha Madimba mkoani Mtwara.*

pili ya mwaka 2017 shirika litakamilisha usambazaji wa mabomba ya gesi kwa matumizi ya majumbani jijini Dar es Salaam na zaidi ya viwanda 300 vimeunganishwa na nishati ya gesi hapa nchini hivyo kupelekea upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Kuhusu upangaji wa bei kwa matumizi ya gesi itakayosambazwa majumbani Mhandisi Musomba anasema Taasisi itashirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati, Maji (EWURA), kuhakikisha nishati hiyo inapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu.

Hivi sasa zaidi ya asilimia 50 ya umeme uliopo katika Gridi ya Taifa unatokana na gesi asilia hivyo mipango ya Serikali ni

kulifanya Shirika hilo kuchangia zaidi mapato Serikalini yanayotokana na rasilimali hiyo.

Mhandisi Musomba Anasema TPDC imejipanga kuwekeza kwenye shughuli za utafutaji, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa gesi ili Taifa linufaikie na rasilimali hiyo.

Akitolea mfano mradi mkubwa wa kusindika gesi asilia (Liquified Natural Gas-LNG), Mhandisi Musomba alifafanua kwamba itachukua takribani miaka 8 hadi 10 kabla ya mzigo wa kwanza wa LNG kusafirishwa kwenda katika soko la dunia kwa mauzo.

Anasema kukamilika kwa mradi wa ***Liquefied Natural Gas- LNG*** utakuwanifursakwa watanzania kupata ajira katika mradi huo

ikiwa ni pamoja na kuchangia pato la mwananchi, wawekezaji na Taifa kwa ujumla.

Anasema uwekezaji katika sekta ya mafuta na gesi ni wa gharama kubwa na hata mafanikio kwa maana ya mapato makubwa kwa Serikali huchukua muda mrefu kuonekana hivyo amewataka wananchi kuwa wazalendo kwa kuilinda miundombinu inayopita maeneo yao.

TPDC inaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ikiwa na lengo la kuongeza uelewa zaidi katika sekta hiyo ya gesi na mafuta.

## Nape: Suala la Utoaji wa Taarifa ni la Kisheria.



**Aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Nape Nnauye akizungumza na Maafisa Mawasiliano wa Serikali wakati akifungua kikao kazi cha 12 cha Maafisa Mawasiliano wa Serikali kinachofanyika Mkoani Dodoma.**

**Na Beatrice Lyimo**

**M**aafisa Mawasiliano Serikalini wametakiwa kuzisoma, kuzielewa na kuzifanya kazi sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na ile ya Haki ya kupata Taarifa ya mwaka 2016 ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika kuuhabarisha umma.

Aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mh. Nape Nnauye anasema ni wajibu wa Maafisa Mawasiliano kuzielewa na kuzitendea kazi Sheria hizo ili kurahisisha upatikanaji wa mawasiliano baina ya Serikali na umma hivyo

## Limeandalowi na Idara ya Habari-MAELEZO

kuondoa ugumu uliokuwepo hususani katika kupatikana kwa taarifa muhimu kwa wananchi," alisema Nape.

Alisema utekelezaji wa sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na ile ya Haki ya kupata Taarifa ya mwaka 2016 utasimamiwa na kuzingatiwa uwepo wa matokeo chanya ya kiutendaji na hivyo kuleta mafanikio makubwa yanayotarajiwa na wananchi juu ya utendaji wa Serikali..

Aliwataka Maafisa Mawasiliano kuwa wabunifu katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuendana na maendeleo ya teknolojia ikiwemo matumizi ya mitandao ya kijamii katika kuhabarisha umma na kutoa taarifa kwa wakati. Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Elisante Ole

Gabriel anawahimiza Maafisa hao kushirikiana na vyombo vyahabari katika kuhabarisha kwa wakati na kuelimisha umma kwa kuzingatia Sheria za nchi ikiwemo Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na kanuni zake.

"Mtahemshimika katika jami endapo mtatoa habari sahihi na kwa wakati; nguvu ya habari ni kubwa, itumieni vizuri kwa kuongeza thamani ya kazi zenu kwa kuhabarisha umma mafanikio ya miradi mbalimbali inayotekelawa na Serikali" alisema Prof. Ole Gabriel.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbasi anasema Serikali itaweka utaratibu maalum wa kupima utendaji kazi

wa kila Afisa Habari katika Wizara, Idara, Taasisi, Wakala na Mamlaka za Mikoa na Wilaya ili kuona ni namna gani ameweza kutoa taarifa za Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya Serikali.

Dkt. Abbas anasema Serikali ya Awamu ya Tano imetekeliza na inatekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kwa kutumia fedha nyingi katika miradi hiyo, hivyo ni wajibu wa Maafisa Habari kueleza wananchi kuhusu miradi hiyo.

Alisema ilitaarifa za utekelezaji wa mafanikio ya Serikali ziweze kuwafikia wananchi, ni wajibu wa Maafisa Habari na Mawasiliano kujenga na kuimarisha mtandao wa mawasiliano baina yao pamojanawatendajiwengine katika maeneo yao ya kazi.



**Aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Nape Nnauye akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa Mawasiliano wa Serikali wakati wa Kikao kazi cha 12 cha Maafisa Mawasiliano wa Serikali kinachofanyika Mkoani Dodoma.**



## DKT.MWAKYEMBE AANZA KAZI RASMI ATOA VIPAUMBELE VYAKE

*Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt Harrison George Mwakyembe na aliyeokuwa  
Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo Mhe. Nape Moses Nnauye wakitia saini hati za  
makabidhiano rasmi ya Ofisi yaliyofanyika katika Ofisi za Wizara Mjini Dodoma*

### Na Raymond Mushumbusi

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe ameanza kazi rasmi ya kutekeleza majukumu kwa kuzungumza na watendaji wa Wizara na wakurugenzi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Katika kikao hicho Dkt. Mwakyembe amesisitiza ushirikiano kati yake na watendaji hao katika kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya wizara.

### Sekta ya Habari

Akielezea vipaumbele vyake katika Sekta ya Habari Mhe. Dkt Mwakyembe amewahakikishia ushirikiano wadau wote wa habari nchini katika kipindi chote ambacho atakuwa katika Wizara hiyo.

Dkt. Mwakyembe pia amewatoa wasiwasi wadau wa habari nchini ambao walikuwa na shaka na hofu juu ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kuwa ni sheria itakayofunga uhuru wa habari bali inadhamira ya kusimamia Sekta ya Habari

### Sekta ya Utamaduni

Kwa upande wa Sekta ya Utamaduni Dkt.Mwakyembe amesisitiza suala la uzalendo kwawananchi katika utendaji wa kazi zetu za ujenzi wa Taifa

Aidha, Dkt Mwakyembe ameleeza kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yazingatiwe.

Ameongeza kuwa katika kipindi chake cha uongozi ataweka msisitizo mkubwa wa kukuza lugha ya Kiswahili ili kukiwezesha kutumika sehemu mbalimbali Duniani.

### Sekta ya Sanaa

Dkt Mwakyembe ameleeza kuwa ataweka mikakati katika kudhibiti wizi wa kazi za ubunifu kwani imekuwa ni tafizo kubwa kwa wasanii nchini kukosa haki za kazi zao.

Ameongeza kuwa yeye akiwa kama mmoja wa waanzilishi wa Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) atalisimamia suala la haki miliki za kazi za sanaa nchini na kuwasaidia kuondokana na kukosa haki za kazi zao.

### Sekta ya Michezo

Katika kikao hicho Dkt Mwakyembe pia alitumia fursa hiyo kuipongeza Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu (Taifa Stars) kwa kushinda mechi zao mbili za kirafiki za kimataifa za Botswana na Burundi zilizofanyika mwishoni mwa mwezi Machi 2017.



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Magufuli akimkabidhi nyenzo za kazi  
Dkt. Harrison Mwakyembe baada ya kumuapisha kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na  
Michezo Ikulu jijini Dar es salaam Machi 24, 2017**

Dkt. Mwakyembe amewaomba wadau wa michezo na watanzania kwa ujumla kuendelea kuipa nguvu na kuisaidia kwa hali na mali Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Vijana chini ya umri wa miaka 17 inayoshiriki katika fainali za mataifa ya Afrika kwa vijana (AFCON) nchini Gabon.

Ameomba wadau wa sekta binafsi nchini kushirikiana na Serikali katika kuendeleza michezo kwani Serikali peke yake haitoweza pasipo ushirikiano kutoka kwa wadau hao.

Aidha, Dkt. Mwakyembe ameahidi kutembelea shule ili kuhamasisha michezo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi.

Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe amechukua nafasi ya Mhe. Nape Moses Nnauye aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo mara baada ya Rais Magufuli kufanya mabadiliko madogo ya Baraza lake la mawaziri hivi karibuni.



**Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo Mhe. Dkt Harrison George Mwakyembe akisalimiana na Naibu wake Mhe. Anastazia Wambura wakati alipowasili katika ofisi za Idara ya Habari (MAELEZO)**

# Sekta ya Filamu kuchangia asilimia 8.7 ya Uchumi wa Taifa ifikapo 2021



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wasanii wa filamu nchini Elizabeth Michael (kulia) na Single Mtambalike (kushoto) walioshinda tuzo za filamu Afrika za mwaka 2016 (African Magic Viewers Choice Award) ziliyofanyika jijini Lagos nchini Nigeria.*

## Na Lilian Lundo

**S**ekta ya Filamu ni moja ya sekta inayokuwa kwa kasi hapa nchini ambapo mpaka sasa sekta hiyo ni ya pili barani Afrika ikitanguliwa na Nigeria katika kuzalisha Filamu.

Sekta hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika uzalishaji wa filamu mbalimbali hapa nchini hasa katika kipindi cha miaka ya 2000 tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya 1970 na 1980 ambapo soko la filamu lilikuwa limetawaliwa na filamu kutoka ughaibuni .

Aidha sababu kubwa iliyosababishwa kukua kwa

sekta hiyo ya filamu hapa nchini ni pamoja na urahisi wa upatikanaji wa vifaa vyta kutengeneza filamu, ongezeko la vituo vya Televisheni za ndani ya nchi ambazo kwa asilimia kubwa watazamaji wake hupenda kufuatilia filamu za Kitanzania.

Ukuaji wa sekta hiyo hapa nchini umetoa ajira kwa vijana wengi wa Kitanzania ambapo baadhi yao wamepata fursa ya kufanya filamu na wasanii wa nje ya Tanzania kama vile nchi ya Nigeria.

Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Joyce Fisoo anasema kwa sasa Sekta ya Filamu ni zaidi ya burudani tofauti na ilivyokuwa miaka ya 70 na 80.

Anasemasektaya Filamu peke yake inatarajia kuchangia asilimia 8.7 ya uchumi wa Tanzania ifikapo mwaka 2021.

Kwa sasa Tanzania ina jumla ya makampuni 139 ambayo yanajihusisha na utengenezaji wa Filamu.

Kwa upande wake, Angelina John mkazi wa Kijitonyama Jijini Dar es Salaam ambaye ni mdau mkubwa wa Filamu za Kitanzania amepongeza juhudini zinazofanywa na waandaajipamoja na wasanii wa Filamu hapa nchini kwa namna wanavyoitendea haki sekta hiyo ambayo inakuwa kwa kasi.



## Na Frank Mvungi

Dhana ya uwajibikaji na kufanya kazi kwa uzalendo ni kichocheo cha maendeleo katika Taifa letu katika kutekeleza dhana ya kujenga uchumi wa viwanda.

Nayasema haya nikirejea kauli ya mwanasheria msomi na nguli wa taaluma ya sheria, Prof. Patrick Lumumba kutoka nchini Kenya ambaye kwa kiasi kikubwa anaunga mkono Juhudi za Rais wetu mpewda, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye kwa hakika amekuwa kielelezaji cha ujenzi wa Tanzania mpya

Nikirejea mahojiano yaliyofanyika hivi karibuni kati ya Prof. Lumumba na moja ya vituo vya luninga hapa nchini msomi huyu anaunga mkono mikakati, mipango na utekelezaji unaofanywa na Serikali ya

Awamu ya Tano unaolenga kuleta mabadiliko makubwa hasa katika kuwainua wananchi wanyonge

"Mimi pamoja na kuwa ni Mkenya lakini ni muumini wa Rais John Magufuli kwa vile anavyoonyesha kwa vitendo dhamira yake ya kuwakomboa Watanzania wanyonge na ni mfano mzuri katika Afrika", alisisitiza Prof. Lumumba

Ni vyema kama Taifa tukajitafakari na kuongeza kasi ya kuunga mkono juhudi za kiongozi wetu mkuu kwa kuwa hata mataifa ya kigeni yanamuunga mkono kwa juhudi zake za kujenga Tanzania yenye uadilifu, uwajibikaji na uzalendo wenye kulenga kuchochea maendeleo ya kila mwananchi na si kundi dogo la watu. Ni katika muda mfupitangu aingie madarakani tumeshuhudia mabadiliko makubwa ya kiutendaji katika utumishi wa

umma na kuongezeka kwa kasi ya uwajibikaji unaolenga kumwinua mtanzania mnyonge.

Tumeshudia Rais Magufuli akipiga vita maadui watatu amba ni rushwa, umaskini na ujinga. Tukitazama maeneo haya matatu tutagundua kuwa ili nchi isonge mbele lazima maadui hawa wapigwe vita na kila mtu pale alipo bila kujali nafasi yake na hapo ndipo Taifa litafikia ustawi wa kweli.

Ziara za mara kwa mara kufuatilia utekelezaji wa maagizo yake ni kielelezaji kuwa Rais Magufuli amedhamiria kutekeleza falsafa ya Hapa Kazi Tu kwa vitendo na huu ni mfano mzuri kwa wote wanaomsaidia Rais Magufuli katika kuwainua Watanzania kiuchumi.

Tumeshuhudia kuanza kwa ujenzi wa barabara za juu katika eneo la Ubungo na Tazara zote zikilenga kuondoa kero ya foleni katika Jiji la Dar es Salaam na mipango mingine kabambe anayoisimamia.

Eneo jingine ni la ujenzi wa reli yenye viwango vya kimataifa (Standard Gauge) kuanzia Dar es Salaam hadi Morogoro kwa awamu ya kwanza, na baadae hadi Dodoma na Mwanza hali itakayopelekea kuwepo kwa mapinduzi katika sekta ya uchukuzi.

Juhudi hizi lazima ziungwe mkono na Watanzania wote kwa kuacha kulalamika na kufanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo ya kweli. Rais Magufuli ameonyesha njia Watanzania tufanye kazi kwa bidii ili tuyafikie maendeleo ya kweli na endelevu.

# TANZANIA MACHII III



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akizungumza baada ya kubaini uwepo wa makontena 20 yenye mchanga wa madini uliokuwa usafirishwe kwenda nje ya nchi.**



**Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akikagua mchanga wa madini alipotembelea mgodi wa dhahabu wa Buzwagi uliopo Kahama mkoani Shinyanga na kuchukua sampuli za mchanga kwa lengo la kwenda kuyapima kwa wataalamu wa madini ili kubaini kiasi cha dhahabu kilichomo.**



**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, akikagua gwaride la Heshima lililoandaliwa kwa ajili yake mara baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa kimataifa wa Mfalme Mswati wa III mjini Mbabane Swaziland Machi 16, 2017 kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa SADC**



**Mhe. George Simbachawene akizindua tovuti za Mikoa na Halmashauri uliofanyika katika ukumbi wa Hazina Ndogo mjini Dodoma. Kulia kwake ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Harrison Mwakyembe.**

# NCHI YETU KATIKA HISTORIA



**Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwasikiliza kwa makini wanafunzi wa kisomo cha watu wazima kwenye kituo cha kati cha kisomo hicho Visiga, kulia ni Mwalimu wa darasa hilo toka Jeshi la Kujenga Taifa Mwaka 1971.**



**Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi akiweka jiwe la msingi katika kiwanda cha kuchambua pamba cha Kakonko Wilayani Kibondo Mwaka 1980.**



**Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa akiangalia mti wa Korosho katika moja ya shamba Wilayani Masasi Mkoani Mtwara.**



**Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akiangalia shamba la mpunga Wilayani Kilosa Mkoani Morogoro.**

# Lugha ya Kiswahili Inahitaji Uwekezaji- Mama Kikwete



**Balozi wa Kiswahili Barani Afrika, Mama Salma Kikwete**

## Na Jovina Bujulu

Balozi wa Kwanza wa Kiswahili Barani Afrika, Mama Salma Kikwete amesema kuwa lugha ya Kiswahili inaweza kutumika katika shughuli mbalimbali ikiwemo kufundishia huku uwekezaji wa kuikuza na kuipanua.

Mama Kikwete aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa Kongamano la Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali, lililofanyika jijini Dar-es Salaam.

Alisema kuwa lugha ndiyo

inayowauunganisha Watanzania na kuwafanya wawe wamoja, hivyo ni wakati muafaka wa kuitumia katika nyanja mbalimbali ili kurahisisha mawasiliano.

Kuhusu suala la lugha ya Kiswahili kutojitosheleza, Mama Kikwete alisema kuwa hilo sio tatizo kwani hakuna lugha yoyote duniani iliyojitosheleza na kutohitaji kukopa baadhi ya maneno.

"Upanuzi wa mawasiliano, na ujenzi wa shule za msingi karibu kila kijiji umefanya watu wasiojua lugha ya Kiswahili kupungua kwa kasi kubwa sana nchini hivyo ni wakati muafaka itumike katika

mawasiliano na kuidumisha, kuikuza ndani na nje ya nchi,"alisema Mama Kikwete.

Naye Dkt. Saidi Sima, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Mwalimu wa somo la Hisabati alisema kuwa Kiswahili ndilo somo sahihi la kufundishia na kueleza uzoefu wake kuwa wanafunzi wengi wanaelewa na kufaulu wanapopewa kazi za masomo kwa kutumia lugha ya Kiswahili na kufanya vibaya kwenye kazi hizo kwa lugha ya Kiingereza.

"Ni vema lugha hii ikapewa nafasi kubwa na kuanza kutumika kufundishia ili kujenga kizazi cha wasomi wanaoelewa wanachojifunza, tofauti na sasa ambapo wengi wao wanahitimu bila kuwa na uelewa wa kutosha juu ya wanachojifunza kutokana na tatizo la lugha" alisema Dkt Sima.

Shyrose Bhanji aliyekuwa Mbunge wa Afrika Mashariki na mdau mkubwa wa lugha ya Kiswahili alisema kuwa Kiswahili kina nafasi nzuri kuwa lugha ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa sababu mpaka sasa nchi tano za Jumuiya hii zinatumia lugha hiyo. Aliendelea kusema kuwa ni muda muafaka wa kuipa heshima lugha ya Kiswahili katika Jumuiya.

# Wawezesheni Maafisa Habari-Simbachawene



## Na Ismail Ngayonga

**W**aziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mhe. George Simbachawene amezitaka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwawezesha Maafisa habari waliopo chini ya Ofisi zao kutekeleza majukumu yao kwa wakatinaharaka ili kuendana na kasi ya ukuaji wa kiteknolojia na kupashana habari ili kuwaleta Wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Simbachawene ameyasema hayo mjini Dodoma wakati akizindua tovuti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zitatumika katika uwasilishaji wa habari na taarifa muhimu kwa Wananchi.

"Nawaagiza Wakuu wa Mikoa wote kuhakikisha Maafisa Habari katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanawanunulia

vifaa hivi muhimu kama kamera, mtandao wa kompyuta, kompyuta na vinginevyo vya kufanya kazi hizi muhimu ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa na kwa gharama ya ofisi ili waweze kuwapatia wananchi taarifa ikiwa ni haki yao ya msingi ya kupata taarifa," alisema Mhe. Simbachawene.

Mhe. George Simbachawene amesema kwa kuwa Tanzania iliweka saini Azimio la 'Open Government Partnership' mwaka 2011, kuweka uwazi wa shughuli za Serikali kwa Wananchi, ikiwa na lengo la kuimarisha Utawala Bora, kuondoa rushwa na kujenga imani kwa Wananchi wake na Azimio linaweka msisitizo kwa Wananchi kupata taarifa kwa wakatinaharaka uhuzaidi.

Aidha Mhe. Simbachawene amewataka Maafisa Habari wa Mikoa na Halmashauri kuhakikisha kwamba tovuti

zao zinakuwa na taarifa sahihi na za kutosha na zinatolewa kwa wakati.

Pia amewataka Watendaji katika Mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa kuondoa urasimu katika kutoa taarifa. "Lazima taarifa zitolewe kwa wakati ili tovuti hizi zitumike kweli kwa malengo yaliyokusudiwa," alisisitiza Mheshimiwa Simbachawene.

Waziri Simbachawene aliwashukuru Watu wa Marekani kuitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani USAID kwa kuwezesha Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma ambao kuitia ufadhilli huo umeweza kuendesha mafunzo ya utengenezaji wa tovuti hizo.

Kwa upande wake Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe aliwataka Maafisa Habari kutowaangusha Wananchi katika kuwapa taarifa pasipo urasimu wowote.

Waziri Mwakyembe amewataka Maafisa Habari kuhakikisha kuwa tovuti hizo zisigeuke kuwa magofu ya habari bali majokofu kwa kupata habari mpya kila siku.

Katika mafunzo hayo, Maafisa habari, na Maafisa Tehama kutoka halmashauri 185 na Mikoa 26 walishiriki Mafunzo hayo na kufundishwa namna ya kuandaa taarifa mbalimbali katika tovuti zao.

# ZIARA YA WAZIRI MKUU WA ETHIOPIA NCHINI



*Waziri Mkuu wa Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia, Hailemariam Dessalegn (kushoto) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli wakipata salamu ya heshima toka kwa kikosi cha Jeshi la Wananchi Baada ya kuwasili nchini hivi karibuni*

*Waziri Mkuu wa Ethiopia Mhe. Hailemariam Dessalegn akiongea na waandishi wa habari katika hafla ya utiliaji saini mikataba ya ushirikiano baina ya Tanzania na Ethiopia, Kulia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ikulu Jijini Dar es Salaam*



*Waziri Mkuu wa Ethiopia, Mhe. Hailemariam Dessalegn (katikati) akifurahia zawadi ya picha ya Bandari ya Dar es Salaam mara baada ya kukabidhiwa na Mwenyekiti wa Bodii ya Wakurugenzi ya TPA, Prof. Ignas Rubaratuka (kulia). Kushoto ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa.*

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli akiagana na mgeni wake Waziri Mkuu wa Ethiopia, Hailemariam Dessalegn kabla ya kupanda ndege na kuondoka jijini Dar es Salaam.*



Welcome to Generation T.Solved

LIMEANDALIWA NA

*Idara ya Habari-MAELEZO  
S.L.P 8031*

*Dar es Salaam-Tanzania  
Simu : (+255) 22 -2122771  
Baruapepe:[maelezo@habari.go.tz](mailto:maelezo@habari.go.tz)  
Tovuti: [www.maelezo.go.tz](http://www.maelezo.go.tz)*



@TZ\_MsemajiMkuu



Msemaji Mkuu wa Serikali



Msemaji Mkuu wa Serikali